

Yuda

Salamu

¹ Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo na nduguye Yakobo:

Kwa wale walioitwa, wapendwa katika Mungu Baba na kuhifadhiwa salama ndani ya Yesu Kristo:

² Rehemaa, amani na upendo viwe kwenu kwa wingi.

Dhambi Na Hukumu Ya Watu Wasiomcha Mungu

³ Wapendwa, ingawa nilikuwa ninatamani sana kuwaandikia kuhusu wokovu ambao tunaushiriki sisi sote, niliona imenipasa kuwaandikia na kuwasihii kwamba mwitetee imani iliyokabidhiwa watakatifu kwa nafasi moja itoshayo.

⁴ Kwa kuwa kuna watu waliojipenyeza kwa siri katikati yenu, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, waovu, wapotoshao neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi wakimkana yeye aliye Bwana wetu wa pekee, Bwana Yesu Kristo.

Hukumu Kwa Walimu Wa Uongo

⁵ Ingawa mmekwisha kujuu haya yote, nataka niwakumbushe kuwa Bwana akiisha kuwaokoa watu wake kutoka nchi ya Misri, baadaye alii-waangamiza wale ambao hawakuamini.

⁶ Nao malaika ambao hawakulinda nafasi zao, lakini wakayaacha makao yao, hawa amewaweka katika giza, wakiwa wamefungwa kwa

minyororo ya milele kwa ajili ya hukumu Siku ile kuu.

⁷ Vivyo hivyo, Sodoma na Gomora na pia ile miji iliyokuwa kandokando, ambayo kwa jinsi moja na hao, walijifurahisha kwa uasherati na kufuata tamaa za mwili zisizo za asili, waliwekwa wawe mfano kwa kuadhibiwa katika moto wa milele.

⁸ Vivyo hivyo, hawa waotao ndoto huutia mwili unajisi, hukataa kuwa chini ya mamlaka na kunena mabaya juu ya wenye mamlaka.

⁹ Lakini hata malaika mkuu Mikaeli alipokuwa anashindana na ibilisi juu ya mwili wa Mose, hakuthubutu kumlaumu, bali alimwambia, "Bwana na akukemee!"

¹⁰ Lakini watu hawa hunena mabaya dhidi ya mambo wasiyoyafahamu. Na katika mambo yale wanayoyafahamu kwa hisia kama wanyama wasio na akili, hayo ndiyo hasa yanayowaharibu.

¹¹ Ole wao! Kwa kuwa wanaifuata njia ya Kaini, wamekimbilia faida katika kosa la Ballaamu na kuangamia katika uasi wa Kora.

¹² Watu hawa ni dosari katika karamu zenu za upendo, wakila pamoja nanyi bila hofu, wakijilisha pasipo hofu. Wao ni mawingu yasiyokuwa na maji, yakichukuliwa na upepo, miti isiyo na matunda wakati wa mapukutiko, ambayo hunyauka, iliyokufa mara mbili na kung'olewa kabisa.

¹³ Wao ni mawimbi makali ya bahari, yakitoa povu la aibu yao wenyewe, ni nyota zipoteazo, ambao weusi wa giza ndio akiba waliowekewa milele.

¹⁴ Enoki, mtu wa saba kuanzia Adamu alitoa unabii kuhusu watu hawa, akisema: "Tazama, Bwana anakuja pamoja na maelfu kwa maelfu ya watakatifu wake,

¹⁵ ili kumhukumu kila mmoja na kuwapatiliza wote wasiomcha Mungu kwa matendo yao yote ya uasi waliyoyatenda, pamoja na maneno yote ya kuchukiza ambayo wenyewe dhambi wamesema dhidi yake."

¹⁶ Watu hawa ni wenyewe kunung'unika na wenyewe kutafuta makosa; wao hufuata tamaa zao mbaya, hujisifu kwa maneno makuu kuhusu wao wenyewe na kuwasifu mno watu wenyewe vyeo kwa ajili ya kujipatia faida.

Maonyo Na Mausia

¹⁷ Lakini ninyi wapenzi, kumbukeni yale mitume wa Bwana Yesu Kristo waliyonena zamani.

¹⁸ Kwa kuwa waliwaambia, "Siku za mwisho kutakuwa na watu wenyewe kudhihaki, watakao-fuata tamaa zao wenyewe za upotovu."

¹⁹ Hawa ndio watu wanaowagawa ninyi, wafuatao tamaa zao za asili, wala hawana Roho.

²⁰ Lakini ninyi wapendwa, jijengeni katika imani yenu iliyo takatifu sana tena ombeni katika Roho Mtakatifu.

²¹ Jilindeni katika upendo wa Mungu mkitazamia kwa furaha rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo ili awalete katika uzima wa milele.

²² Wahurumieni walio na mashaka;

²³ wengine waokoeni kwa kuwanyakua kutoka kwenye moto; nao wengine wahurumieni mkiwa na hofu, mkichukia hata vazi lenye mawaa na kutiwa unajisi na mwili.

Dua Ya Kutakia Heri

²⁴ Kwake ye ye awezaye kuwalinda ninyi
msianguke na kuwaleta mbele za utukufu wake
mkuu bila dosari na kwa furaha ipitayo kiasi:

²⁵ kwake ye ye Mungu pekee Mwokozi wetu,
kwa Yesu Kristo Bwana wetu, utukufu, ukuu,
uweza na mamlaka ni vyake tangu milele, sasa
na hata milele! Amen.

**Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia
Takatifu™ (Bible)**

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 18 Apr 2025 from source files dated 31 Aug 2023

9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462